



SMT, SMZ zashirikiana utatuji sekta ya mifugo

Na Paul Mabeja, DODOMA

KAIMU Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Charles Mhina, amesema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (SMT) na ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), zinashirikiana kutatua kero zilizoko katika sekta ya mifugo ili kufikia uzalishaji wenyewe tija.

Alibainisha hayo juzi wakati aki fungua kikao cha ushirikiano kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muun-

gano wa Tanzania (SMT) na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) kilichofanyika mkoani hapo.

“Tumekuwa tukishirikiana pia kwenye maeneo ya masoko kuona ni namna gani tunaweza tukaimarisha masoko ya bidhaa za mifugo kwa pande zote mbili.

Kwa hiyo ushirikiano huu unalenga kuondoa vikwazo ambavyo vinaweza kuifanya biashara ya mifugo isikue kwa haraka,” alisema Dk. Mhina.

Dk. Mhina alisema sehemu zote za bara na Zanzibar kuna viwanda

vya kuzalisha bidhaa za mifugo ikiwamo nyama, ngozi, maziwa na bidhaa nyingine, hivyo ushirikiano huo utasaidia kuimarisha sekta ya mifugo.

Alisema ushirikiano huo umelenga kutatua kero kwenye maeneo mbalimbali hususani za kiko di kwa kushauri mamlaka husika ziweze kufanya marekebicho, ili kuwezesha biashara kufanyika kwa urahisi zaidi kati ya pande zote mbili za muungano.

Aidha, alibainisha kuwa ushirikiano huo utajikita katika

maeneo ya utafiti na mafunzo ili waweze kujifunza kila upande ni namna gani sekta zinafanya ili kuzalisha kwa tija mifugo na bidhaa zake.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, Dk. Omary Ali Amir, alisema wanatumia ushirikiano huo kujifunza tafiti mbalimbali na pia kujenga uwezo wa wataalamu wao kupitia Tanzania Bara kwa kuwa wako mbele kwenye masuala mengi ikiwamo uzalishaji, masoko na utafiti.

majawabu.

Njombe.

Alisema kicheni pati pia

watoto wao pasipo kujali jinsia zao.

taendelea kuheshimu misingi ya ndoa zao hasa waume zao.

HABARI LEO UK 4.

CCM yataka sensa ya mifugo

Na Ikunda Erick, Simanjiro

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) kimeilagiza Wizara ya Mifugo na Uvuvi ifanye sensa ya mifugo hasa ng'ombe ili kufahamu kama waliopo wanaendana na eneo la ardhi ya malisho.

Katibu Mkuu wa CCM, Daniel Chongolo alitoa agizo hilo katika Kijiji cha Naisinyai wilayani Simanjiro akiwa kwenye ziara kukagua utekelezaji wa ilani ya

uchaguzi ya chama hicho mkoani Manyara.

"Ni wakati mwafaka kwa Wizara ya Mifugo kuendesha sensa ya mifugo ili kufahamu mlinganyo wa mifugo tulionayo na ardhi iliyopo, ili itafutwe suluhu ya kuhimili migogoro ya ardhi, kama ni mingi tujue itapunguzwaje na kama ni midogo iongezwe," alisema.

Katika hatua nyingine, alikagua mradi wa maji wa Meshie kwenye Kata ya Mirerani na kueleza changamoto ya upa-

tikanaji wa mawasiliano ya simu kwa kuwa hakuna minara.

Chongolo alisema upo Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (UCSAF) ambao hadi sasa umejenga minara kwa fedha za serikali.

"Nachukua changamoto hiyo ya mawasiliano ninaenda kumpatia Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye ambaye hivi karibuni alikuwa Longido mkoani Arusha akisimika mnara wa mawasiliano," alisema.

Alisema Nape anafanya kazi

nzuri hivyo atawasiliana naye ili wananchi wa maeneo hayo nao wapate huduma ya mawasiliano.

Nape alisema serikali inafanya kazi ili ambako kampuni za simu zinashindwa kufika kutokana na sababu mbalimbali inabeba jukumu hilo ili kuwapa wananchi unafuu wa maisha.

Chongolo yupo mkoani Manyara kwa ziara ya kikazi akifuatana na Katibu wa Halmashauri Kuu (NEC), Itikadi na Uenezi, Sofia Mjema na Katibu wa NEC, Oganaizesheni, Issa Gavu.